


HALMASHAURI YA WILAYA KISARAWE



29 Juni, 2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Kisarawe anakaribisha maombi ya kazi kwa watazania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya Watendaji wa Kijiji.

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA III - NAFASI 4

SIFA ZA MWOMBAJI -

Awe mwenye elimu ya kidato cha nne au sita aliyehitimu mafunzo ya astashahada/cheti (NTA level 5) katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika chuo cha serikali za mitaa Hombolo, Chuo cha Dodoma au chuo chochote kiinachotambuliwa na Serikali.

Ngazi ya Mshahara TGS B

MAJUKUMU YA KAZI

- I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- II. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao. Kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika kijiji.
- III. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji.
- IV. Kuratibu Mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- V. Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu za uendeshaji wa Serikali ya Kijiji.
- VI. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- VII. Kiongozi wa wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika kijiji.
- VIII. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
- IX. Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo katika kijiji.
- X. Kupokea, kusikiliza kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- XI. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji na
- XII. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

MASHARTI YA JUMLA

Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.


1. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
2. Waombaji watalazimika kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
3. Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingialia katika kada tofauti walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao.
4. Waombaji waabatanishe maelekezo binafsi yaliyojitosheleza (detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (3) wa kuaminika.
5. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma na vyeti vya kidato cha nne au sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia kazi husika. Pia ambatanisha picha ndogo (passport size moja) ya hivi karibuni ndani ya miezi mitatu na iandikwe jina nyuma yake.

6. Testimonials, provisional results, statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (form VI and IV results slips) HAVITAKUBALIKA.
7. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika (NECTA, NACTE na TCU).
8. Waombaji waliofukuzwa kazi katika utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
9. Uwasilishaji wa sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua stahiki za kisheria.
10. Maombi yaandikwe kwa mkono na muombaji kwa lugha ya kishwahili au kiingereza.
11. Waombaji wote kwenye barua zao za maombi waandike namba za simu za uhakikia kwa ajili ya mawasiliano.
12. Maombi yote yatumwe kwa anuani ya posta kama ifuatavyo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe,
S.L.P 28001,
KISARAWA.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20 Julai, 2021 saa 9.30 Alasiri.

Limetolewa na


Mussa L. Gama
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWA.

Nakala: Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320,
DODOMA.